



United Nations  
Educational, Scientific and  
Cultural Organization

## **Ujumbe kutoka kwa Bi. Irina Bokova, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Tarehe 5 Juni 2017.**

**Kuunganisha Watu na Asili**

Inaweza kuwa vigumu kuamini sasa, lakini miaka hamsini iliyopita ilidhaniwa kuwa njia bora ya kulinda asili ni kuiweka mbali na watu ...

Hii leo, tunajua vyema zaidi.

Sasa tunajua kuwa kadri uhusiano baina ya watu na mazingira yao unavyokuwa wa karibu zaidi ndivyo watu wanavyofahamu zaidi juu ya umuhimu wa asili na viumbe hai, urithi na maji, kwa ajili ya ustawi wao binafsi na kwa ajili ya hali ya baadaye ya sayari yetu.

Msukumo huu huongoza hatua zote za UNESCO kama ilivyo katika upekee wa mtandao wa kimataifa wa maeneo yake teule na kama iliyoundwa katika kuleta watu karibu na asili, kuchora ramani mpya ya dunia - ramani ya umoja na amani, iliyo zaidi ya mipaka ya kawaida, baina ya wanawake na wanaume na mazingira yanayowazunguka.

Hifadhi za Bayongahewa za UNESCO, maeneo ya hifadhi ya jiorojia ya UNESCO na maeneo ya Urithi wa Dunia – yanayotegemea mara nyingi maji yaliyo juu au chini ya uso wa dunia – hufanya jumla ya hifadhi za kipekee zilizo zaidi ya 2,000 duniani kote. Maeneo hayo hutoa ajira kwa watu wanaoyazunguka na milango yake iko wazi kwa umma wote, kwa sababu sasa tunajua kuwa hii ndio njia ya uhakika zaidi ya kufikia maendeleo shirikishi na endelevu na inayoheshimu mipaka ya sayari yetu. Maeneo ya hifadhi ya jiorojia ni vitabu vilivyvyo wazi vya kihistoria ambavyo huturudisha nyuma mamilioni ya miaka. Hifadhi za Bayongahewa ni mahali ambapo jamii hukabiliana na changamoto za maendeleo kwa kuunda njia mpya za kijamii na uchumi endelevu. Maeneo ya hifadhi ya jiorojia na hifadhi za bayongahewa huunganisha uhifadhi na elimu kwa mbinu mpya ya maendeleo endelevu, kama vile utalii wa mazingira na kilimo hai.

Yote haya huongozwa katika eneo husika, lakini maeneo haya yako ndani ya mtandao wa kipekee wa kimataifa unaouruhusu kushirikishana mawazo, uzoefu na mbinu bora kwa upana zaidi. Kuheshimu mazingira ya asili hutokana na uelewa, ndio maana UNESCO ilizindua kivunge cha elimu ya viumbe hai kwa watoto wa shule.

Maji huunganisha watu na asili, na maeneo ya UNESCO ya Urithi wa Kitamaduni wa Ulimwengu ni mifano ya jinsi binadamu alivyoweza kusimamia maji ili kuyapata, kuyatunza, kutumia nguvu zake na kuyahifadhi. Hauhitaji kutafuta zaidi ya mifereji maalumu ya maji, bustani za maji na viwanda ambavyo ni alama kwa mandhari yetu.

Leo, ninamkaribisha kila mmoja kutenga muda binafsi na kutembelea moja ya maeneo hayo ya UNESCO. Kupitia katika tafakari ya kina; jitumbukize katika Bustani ya Kiajemi ya Iran ambako maji hufanya ishara za maumbo ya mapambo mbalimbali. Huko katika eneo la hifadhi ya jiorojia la UNESCO la Tumbler Ridge ya huko Canada, ogelea katika maziwa ya Alpine yenye maji angavu kama kioo na kulala chini ya nyota. Au fanya safari ya kutembea kwa miguu katika hifadhi ya Bayongahewa ya Mujib huko Jordan ambayo ipo mita 420 chini ya usawa wa bahari, shukrani kwa ukaribu wake na Bahari ya Chumvi.

Katika hii Siku ya Mazingira Duniani, ninatoa wito kwa nchi zote kutumia ipasavyo maeneo haya teule ya UNESCO – zaidi ya yote, ninatoa wito kwa wanawake na

wanaume kila mahali kuungana na asili inayowazunguka na inayoleta uzuri, maana na amani katika maisha tunayoishi.